**SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI**

**WAKALA YA BARABARA**

## TAARIFA YA NYARAKA ZA NYENZO ZA USIMAMIZI WA MASUALA YA MAZINGIRA NA JAMII KWA MRADI WA MABASI YAENDAYO HARAKA AWAMU YA NNE (4)

Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) kwa niaba ya Wizara ya Ujenzi inakusudia kuanza ujenzi wa Barabara ya mabasi yaendayo haraka awamu ya nne, Lot 1; Road works 13 km (From CBD Maktaba ya Taifa to Mwenge /Ubungo (Sum Nujoma)) and Lot2; Road works 15.63km (From Mwenge to Boko Basihaya (Dawasa)) Mkoani Dar es Salaam.

Benki ya Dunia wameonesha nia ya kufadhili mradi huu kupitia Mradi wa mabasi yaendayo haraka awamu ya nne.

Kwa kuzingatia matakwa ya Muongozo wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Jamii wa Benki ya Dunia, Wakala ya Barabara (TANROADS) imeandaa Nyenzo za Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Jamii zikiwemo: (i) Ahadi za Utekelezaji wa Masuala ya Mazingira na Kijamii; (ii) Mpango wa Usimamizi wa Masuala ya Mazingira na Kijamii; (iii) Mpango wa Ushirikishaji wa Wadau; (iv) Mpango wa Usimamizi wa Wafanyakazi; (v) Mpango mkakati wa Kushughulikia Masuala ya Unyanyasaji wa Kijinsia; (vi) Muongozo wa Upangaji wa Vikundi Vilivyo Katika Mazingira Hatarishi; na (vii) Sera na Muongozo wa Uhamishaji wa Makazi, kwa ajili ya kuongoza utekelezaji wa mradi.

Kwa Tangazo hili, Wakala ya Barabara inaweka wazi taarifa hizi na inawaalika wadau na umma kwa ujumla kuipitia kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa masuala ya mazingira na jamii wakati wa utekelezaji wa mradi hiyo.

Aidha, Umma unaweza kuona taarifa hizi kwenye Tovuti ya TANROADS: **www.tanroads.go.tz,** Tovuti ya Benki ya Dunia; **worldbank.org** na kwenye ofisi zifuatazo:

1. Tanzania National Roads Agency (TANROADS)
   P.O. Box 11364
   10 Shaaban Robert Road/Garden Avenue Junction
   **Dar es Salaam.**
   Email: tanroadshq@tanroads.go.tz

2. TAN ROADS- Dar es Salaam Regional Office
   P.O. Box 4838
   **Dar es Salaam.**
   Email:rm-dsm@tanroads.go.tz